NIPASHE UK7.

# Serikali kuanzisha kampeni chanjo wanyama wafugwao

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdalah Ulega (pichani), amesema serikali inatarajia kuanzisha kampeni ya lazima ya chanjo kwa wanyama wafugwao nyumbani.

Amesema hatua hiyo itasaidia kupunguza au kuondoa hatari ya asilimia 70 ya magonjwa ya milipuko kwa binadamu yanayotoka kwa wanyama.

Waziri Ulega alisema hayo jana alipotembelea Hospitali ya Taifa ya Rufani ya Wanyama iliyoko Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) wakati wa maadhimisho ya 18 ya kumbukizi ya Hayati Edward Moringe Sokoine yanayofanyika chuoni hapo kuanzia jana hadi Ijumaa.

Alisema kwa sasa nchi inapaswa kuingia kwenye kampeni ya kuchanja mifugo ya kufugwa itakayosaidia kupunguza magonjwa ya milipuko kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu.

Ulega alisema kuna umuhimu mkubwa wa kuzingatia sera ya kuchanja kwa wanyama wafugwao kama ilivyo kwa binadamu kwa sababu karibu asilimia 70 ya magonjwa ya binadamu yanatoka kwa wanyama hasa wanyamapori ikiwamo Corona, Murburg, kimeta, homa ya mgunda.

Alisema kampeni ya kuchanja pia itasaidia kutoa ajira za muda mrefu na mfupi kwa wataalamu wa wanyama walioko nchini sambamba na vijana wanaosoma kwenye vyuo mbalimbali kutumia nafasi hiyo kujifunza kwa vitendo na nchi kupata wataalamu wengi zaidi wa masuala ya wanyama.

Aidha, Ulega alisisitiza vijana na wawekezaji nchini kuhakikisha wanajikita katika kilimo cha majani ya malisho ya mifugo kwa ajili ya biashara hasa majani aina ya Apha -alpha kutokana na majani hayo kuwa na masoko zaidi ya ndani na nje ya nchi ikiwemo nchi ya Saudi Arabia.




Akizindua maadhimisho hayo, Ulega alisema serikali imelenga kuwahamasisha vijana kujihusisha na shughuli za ufugaji kibiashara kwa kuanzisha vituo atamizi vinane kwa ajili ya vijana, huku ikipanga kuongeza vingine vinane kwa mwaka ujao wa fedha 2023/24 sambamba na kuiwezesha kampuni ya Ranchi ya Taifa (NARCO) kuzalisha chakula bora cha mifugo, kuzalisha ndama bora na kuboresha majike wazazi.

Alisema ikiwa vijana watajiunga na shughuli za ufugaji kibiashara itawasaidia sababu malighafi katika viwanda vya nyama nchini, itakuwa imeongezeka na kutoa fursa ya kujiajiri na kisha kuchangia katika maendeleo ya Taifa.

Aidha, alitoa wito kwa sekta binafsi na washirika wa maendeleo kuendelea kujitokeza na kuunga mkono katika kuwawezesha vijana kushiriki kwenye shughuli za kilimo kwa kutoa msaada wa hali na mali ikiwemo mitaji ya fedha, vitendea kazi, mafunzo na teknolojia zitakazowawezesha kushiriki katika kilimo kwa tija na ufanisi.





# Waomba kikosi maalumu kudhibiti uvuvi haramu

**Na Rose Jacob,** UKEREWE

BAADHI ya wananchi wilayani Ukerewe mkoani Mwanza, wameiomba serikali kupeleka kikosi maalumu kwa ajili ya kukabiliana na uvuvi haramu.

Wamesema wanaohusika ni baadhi ya watu wakiwamo viongozi wa ngazi mbalimbali hali inayosababisha upungufu wa samaki.

Walieleza hayo kwa nyakati tofauti baada ya kupigwa marufuku kwa baadhi ya mitego inayotumika kinyume cha sheria katika Ziwa Victoria yakiwamo makokolo.

Makokolo hayo yamekuwa yakikamatwa na kufikishwa pungufu katika maeneo husika kutokana na wamiliki wake kuwa miongoni mwa viongozi wa ngazi mbalimbali serikalini.

**Wanaohusika ni baadhi ya watu wakiwamo viongozi wa ngazi mbalimbali hali inayosababisha upungufu wa samaki.**

Mkazi wa Nansio, Suzaba Mafuru: “Tunaiomba serikali kuwachukulia hatua kali watumishi wa umma wanaojihusisha na vitendo vya uvuvi haramu maana wao wamekuwa chanzo cha hali hiyo kuwa endelevu, vifaa vikikamatwa kwa ajili ya kuteketezwa wanatunza na kupeleka vichache na uvuvi huo unaendelea ni bora kiwepo kikosi maalumu ambacho kitakuwa msaada juu ya tatizo hili.”

Aidha waliiomba serikali kuwa na utaratibu wa kuwahamisha kila baada ya muda watumishi wa sekta ya uvuvi kutokana na viongozi wa idara hizo kuyazoea mazingira baada ya kutumika maeneo husika kwa kipindi kirefu.

Nao baadhi ya madiwani wa halmashauri hiyo wakizungumza wakati wa kikao cha kawaida walisema hali ya udhibiti uvuvi haramu bado iko chini hivyo kuishauri serikali itenge watu maalumu watakao pambana na suala hilo.

“Maofisa uvuvi wamezidiwa na jukumu hilo hivyo kusababisha uvuvi haramu, unaoua samaki wachanga na mazalia ya samaki ambayo yakitoweka yataleta shida ya uchumi kwa wananchi na serikali kwa ujumla maana hiki ndicho chanzo chetu kikuu cha uchumi,” alieleza Diwani John Ndaro.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Joshua Manumbu, alisema Chama Cha Mapinduzi (CCM) na serikali wawe nguzo kuu ya kupambana na uvuvi haramu na kueleza kuwa kuna baadhi ya viongozi wanamiliki makokolo.

Alisema baadhi ya viongozi hao wamewapa ndugu zao makokolo, wanayatumia katika uvuvi.



N
k
n
Za
Zi
K

**Na Vi**

BARA
Mazi
gozi
fuata
wataf
Hat
fanyil
shugh
stareh
kiwar
hapa.

# Wizara yakanusha nyama kuua watu watatu Rombo

**Na John Nditi, Morogoro**

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imesema vifo vya watu watatu vilivyotokea katika kata ya Kisale Msaranga wilayani Rombo katika Mkoa wa Kilimanjaro havina uhusiano na ulaji wa nyama.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Profesa Riziki Shemdoe alisema mjini Morogoro baada ya kusaniwa kwa mashirikiano kati ya taasisi 11 zilizochini ya wizara hiyo na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA).

Profesa Shemdoe aliwaeleza waandishi wa habari kuwa baada ya kuripotiwa na vyombo vya habari kuwa watu hao walifariki dunia baada ya kula chakula msibani, timu ya wataalamu wa Kanda ya Kaskazini kupitia vituo vyake vya maabara ya veterinari Tanzania (TVLA) vilichunguza suala hilo.

"Taarifa tuliyonayo waliyotupatia wataalamu wetu ni kwamba vifo vile havina uhusiano wowote na ulaji wa nyama kama iliyoelezwa," alisema Profesa Shemdoe.

Alisema tayari wenzao wa idara ya afya wamechukua sampuli kwa wale wanaojisikia vibaya ili kufanya utaratibu wa kuchunguza kinachoendelea.

Hivi karibuni kulikuwa na taarifa za watu watatu wakazi wa kata ya Kisale Msaranga, Wilayani Rombo mkoani Kilimanjaro kufariki dunia muda mfupi baada ya kula chakula msibani.

Taarifa zilidai kuwa kabla ya vifo hivyo watu hao waliharisha, walitapika, walitokwa na makamasi yenye damu na walisikia maumivu ya mgongo na kichwa.

HABARI LEO UK 17.

# Ulega: Chanjo kwa mifugo si hiari, ni lazima

Na John Nditi, Morogoro

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi , Abdallah Ulega amesema chanjo kwa mifugo sio la hiari tena, bali ni lazima ili kudhibiti magonjwa yanaoambukiza kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu.

Pia, ameeleza kuwa hatua hiyo itaongeza mauzo ya nyama nje ya nchi kutoka tani 12, 000 za sasa na kufikia tani 50,000 hadi 100,000 kwa mwaka.

Ulega alisema hayo juzi katika hotuba yake ya ufunguzi wa kumbukizi ya 18 ya Hayati Edward Moringe Sokoine ya kutimiza miaka 39 tangu kifo chake kilichotokea Aprili 12, mwaka 1984 eneo la Wami Ruhindo, wilayani Mvomero, mkoani Morogoro.

Chuo Kikuu hicho kilisongeza mbele maadhimisho ya kumbukizi yake kutoka Aprili 12, mwaka huu na kupangwa kuadhimishwa kuanzia Mei 23 hadi 26, mwaka huu.

Ulega alisema asilimia 70 ya magonjwa ya binadamu yanatoka kwa wanyama na hasa wanyamapori.

Alisema ili kukabiliana na changamoto hizo upo umuhimu wa kuchanja wanyama hasa wale wanaofugwa.

"Ndiyo maana kwa sasa tunakwenda na ule mkakati wa lazima ya kuchanja" alisisitiza Ulega

Alisema kutokana na changamoto hiyo Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kupitia Hospitali yake ya Rufaa ya Taifa ya wanyama imekuwa ikihakikisha inafanya tafiti nyingi ili kukabiliana na magonjwa hayo kwa kushirikiana na serikali.

Alisema Chuo Kikuu hicho kimekuwa na mchango mkubwa katika kukabiliana na magonjwa yanayoibuka kwa wananchi kutokea kwa wanyama na hivyo serikali haina budi kuchukua hatua za kuwakinga binadamu pamoja na wanyama wenyewe.

Kwa mujibu wa Ulega katika kukabiliana na changamoto hizo zinazojitokeza nchini, serikali imeweka sera nzuri ya Afya Moja.

Alisema ni muhimu kwa wataalamu na viongozi wa serikali na taasisi nyingine kusimamia kikamilifu mpango wa afya moja ili kuzuia na kuthibiti magonjwa hayo kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu .

Kwa upande wake, Makamu mkuu wa Chuo cha SUA, Profesa Raphal Chibunda alisema kwa sasa wanao ushirikiano na Maabara ya Taifa ya Mifugo na maabara zilizopo wanafanya kazi kwa karibu za utafiti wa magonjwa ya wanyama na kutoa majibu .

Serikali kuweka mazingira bora ya vipaji

CamScanner

# Livestock vaccination made mandatory

**From DAILY NEWS Reporter in Morogoro**

LIVESTOCK vaccination is now mandatory, the government has announced as part of measures to prevent transmission of zoonotic diseases.



*ABDALLAH Ulega*

The Minister for Livestock and Fisheries, Abdallah Ulega, said in Morogoro yesterday that apart from preventing transmission of zoonotic diseases, mandatory vaccination would also help to boost annual meat export from the current 12,000 tonnes to between 50,000 and 100,000 tonnes.

"Vaccination is a crucial step in the prevention of infections in both the people and animals, said the minister at the beginning the 39th death anniversary of former prime minister, Edward Sokoine, who passed away on April 12, 1984, in Wami Ruhindo, Mvomero District, Morogoro Region.

According to him, animals, especially wildlife, are the reason for roughly 70 per cent of human ailments.

Mr Ulega added that vaccination aids in triggering an immune response without actually transmitting the disease.

He stated that the Sokoine University of Agriculture (SUA) has continued to make efforts to ensure that it carries out several studies to address animal ailments in partnership with the government through its Animal Referral Hospital.

Mr Ulega said zoonotic diseases caused by animals include the Marburg Virus Disease (MVD), an anthrax disease that affects cows, donkeys, sheep, goats and horses), people can get sick with anthrax if they come in contact with infected animals or contaminated animal products.

In addition to that, another disease is leptospirosis, a bacterial disease that affects humans and animals.

He said the government has put in place the One Health approach as a major strategy of disease control and prevention as it emphasizes the relatedness of human, animal, and environmental health as well as the importance of trans - disciplinary efforts to control emerging pandemic threats.

He said the ministry has a mission to conduct a campaign to vaccinate livestock in the country and to coordinate the vaccination of livestock throughout the country in accordance with the calendar.

More than 200 SUA students will participate in the immunisation campaign and travel throughout the country to carry out the task, which will go beyond their practical training and allow them to contribute to their country, according to Ulega.

For his part, Prof Raphael Tihelwa Chibunda, Vice-Chancellor of SUA, stated that their laboratory closely works with the Tanzania Veterinary Laboratory Agency (TVLA) to investigate animal ailments and propose solutions.

According to him, the university's laboratory at the SUA animal referral Hospital receives parasite samples from TVLA and the two organisations work together to diagnose the issue there.

## Relief as lion

